

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



16 Mtaa wa Urambo,  
Simu Nambari: 2150043 – 6/2150360  
Fax No: (022) 2150047  
SALAAM  
E-mail: [dgeneral@pccb.go.tz](mailto:dgeneral@pccb.go.tz)  
Website: [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

---

**MHANDISI WA TANESCO AFIKISHWA MAHAKAMANI**

Mhandisi wa Shirika la Umeme - TANESCO Makao Makuu, Stanslaus Simbila amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Jumanne tarehe 09/10/2018 mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mheshimiwa Hamza, kwa kosa la Matumizi Mabaya ya Ofisi, kinyume na Kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007.

**Ufafanuzi wa tuhuma:**

Mshitakiwa anadaiwa kutenda kosa wakati akiwa Meneja Mradi (Project Manager) katika mradi namba **PA/001/08/HQ/G/123** uliokuwa ukitekelezwa kati ya TANESCO na Kampuni ya Zwart Technick B.V ya Uholanzi. Mradi huo ulihusu ufungaji wa Majenereta ya kufulia Umeme katika miji mitano ya Sumbawanga, Kigoma, Kasulu, Kibondo na Loliondo.

Inadaiwa kuwa Mshitakiwa akiwa *Project Manager* alitoa *completion certificate* na *operational acceptance certificate* zilizopelekea kiasi cha **Euro 491,622.42** kulipwa kwa Kampuni ya Zwart Techick B.V kabla ya kumaliza kazi zilizokuwa zinatakiwa kukamilishwa ikiwa ni pamoja na kuhaifanya kazi hiyo chini ya kiwango kilichokusudiwa. Kosa hili ni ni kinyume na Kanuni ya 123 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2005.

Mshitakiwa amekana kutenda kosa hilo na yuko nje kwa dhamana baada ya kutimiza masharti yote yaliyoweka na Mahakama kuhusu dhamana yake. Kesi hiyo itatajwa tena **Tarehe 08/11/2018** kwa ajili ya kupanga siku ya kusoma maelezo ya awali.

**IMETOLEWA NA OFISI YA AFISA UHUSIANO, TAKUKURU MAKAO MAKUU  
10/10/2018**